

# Kuelekea Pentekoste... Njoo Roho Mtakatifu!


Tarehe 8 Juni tutaadhimisha sikukuu kubwa ya **PENTEKOSTE**…Matukio ya sasa, kwa Kanisa, tayari yanatuweka katika ombi hili kubwa la Roho Mtakatifu, la nuru yake na la Mapaji yake : *hekima, akili, nguvu, elimu, shauri, ibada na uchaji wa Mungu*. Mapaji yanayotualika kuamini, na kwamba wote tunapaswa kuomba tayari kwa ajili ya Papa wetu ajaye.

**Papa ni mrithi,** siyo wa yule au wale waliomtangulia, bali wa **PETRO,** yule ambaye Yesu alimwambia ***« wewe ndiwe Petro na juu ya mwamba huu nitalijenga kanisa langu »*** Mathayo 16 :13-20. Papa ambaye atachaguliwa kwenye Mkutano wa makadinali, kuanzia tarehe 7 Mei, atakuwa mrithi wa PETRO, ambaye alichaguliwa na Kristo karibu na ziwa Tiberia… **Roho Mtakatifu** atatupilia mbali orodha za « mapapa » ambazo hujadiliwa mara kwa mara kwenye vyombo vya habari, kwa njia ya kisiasa zaidi kuliko ya kikatoliki !!…



Kwa bahati nzuri, ni Yeye ambaye anafanya kazi ndani ya moyo wa Kanisa, tunahitaji tu kuwa waaminifu kwake…na watulivu ! Nasi tutamkaribisha papa wetu mpya kwa imani na furaha, tukiomba kwamba Roho Mtakatifu amwongoze, na Bikira Maria amsindikize kama alivyofanya kwa mitume.

## 19 na 22 Juni SIKUKUU YA MWILI NA DAMU YA KRISTO.



### Sikukuu ya Sakramenti Takatifu

**Tushukuru kwa uwepo halisi wa Kristo kati yetu.**

>> **BARUA PEPE**.

« **Ekaristi, katika maisha yangu,** ni Nuru inayotuongoza,
mti wa Maisha, **Jua la Maisha**, hazina yenye thamani zaidi kwangu.
Ni nuru yangu katika giza. Asante Petro Vigne.» I.B. Burgos. Uhispania

Baada ya kusoma « *Neno la Petro Vigne kwa Leo* », nimetambua kwamba **Petro Vigne alipenda Ekaristi Takatifu** na misa Takatifu aliyoiadhimisha kwa uangalifu mkubwa. Ninamshukuru sana Mungu kwa ujumbe mzito ninaoupata kupitia Mwenyeheri Petro Vigne. *Neno la Petro Vigne* limenifanya kupenda adhimisho la misa na nimependa hasa muda wa kutubu dhambi… wakati tunapoimba Mtakatifu… naona kwa hakika Ukuu wa Mungu, Utakatifu wa Mungu,… Muda wa mageuzo, *Neno la Petro Vigne kwa leo* limeniwezesha kuelewa ukuu wa Mungu anayeshuka juu ya altare katika maumbo ya mkate na divai kwa mikono ya Padre, Yesu mwenyewe anashuka ndani ya roho yangu. Kwa ujumla, **shukrani kwa Petro Vigne,** nimeelewa kwamba misa takatifu ni makutano kati ya Mungu na mwanadamu. Tuendelee kumwomba Mwenyeheri Padre Vigne atuombee ili tuelewe vizuri thamani ya Misa Takatifu. Amino Linus Shawa Morogoro TANZANIA

**WATAWA WA SAKRAMENTI TAKATIFU**
NYUMBA MAMA : 113, AVENUE VICTOR HUGO 26000 VALENCE - UFARANSA

N° 05-06. 2025
*Imetolewa: Shirika la Masista wa Sakramenti Takatifu*

# NENO
Mwenyeheri PETRO VIGNE Leo



# Katika mwanga wa Pasaka

Ni kawaida kwamba namba hii itiwe alama na kifo cha PAPA wetu FRANSISKO na ambaye kupitia maandishi yake mwenyewe tunaweza kuonesha **ASANTE yetu kwa miaka 12 na siku 39 iliyotolewa kwa huduma ya Kanisa**

Tutaendelea kuwasilisha ujumbe wako uliotufikishia kupitia matendo na mitazamo yako, bila shaka… bila kusahau yale uliyotuachia kupitia ensiklika zako : **Lumen Fidei** : Mwanga wa Imani ;
**Laudato Si'** :juu ya kutunza nyumba yetu ya pamoja;
**Fratelli Tutti** :juu ya undugu na urafiki wa kijamii ;
**Dilexit nos** : juu ya upendo wa kibinadamu na wa kimungu kutoka moyoni wa Yesu-Kristo.



Tarehe 19 Aprili 2025, katika mkesha wa Pasaka ulituambia *:*

**Maisha yetu yote yanaweza kuwa uwepo wa matumaini.** Tunataka kuwa hivyo kwa ajili ya wale wasio na imani kwa Bwana, kwa ajili ya wale waliopoteza njia yao, kwa ajili ya wale waliokata tamaa au walio na migongo iliyopindana chini ya mizigo ya maisha, kwa ajili ya wale walio peke yao au waliofungwa katika mateso yao, kwa ajili ya maskini wote na wanaokandamizwa wa duniani, kwa ajili ya wanawake wanaofedheheshwa na kuuawa, kwa ajili ya watoto ambao hawajazaliwa na wale waliotendewa vibaya, kwa ajili ya wahanga wa vita. **Kwa wote na kwa kila mmoja, tubebe matumaini ya Pasaka!**

**… Tutengeneze nafasi kwa ajili ya nuru ya Yeye aliyefufuka!** Na tutakuwa wajenzi wa matumaini kwa ajili ya ulimwengu.

Dada, na kaka, katika ajabu ya imani ya Pasaka, tukibeba ndani ya mioyo yetu matarajio ya amani na ya ukombozi, tunaweza kusema :
**Pamoja nawe, Bwana, yote ni mapya.**
**Pamoja Nawe,**
**Yote yanaanza upya**
.

⇧ Na sentensi ya mwisho ya homilia yako ya jumapili ya pasaka. .

# Asante kwa Papa wetu Fransisko

Kwa ajili ya safari yetu ya kipindi cha Pasaka tunakaribisha bado jumbe zako :

Nuru ya Yesu inang'ara, kwenye nyuso za wakristo, kama katika kioo, na hivyo inaenea na kutufikia, ili nasi tuweze pia, kushiriki katika maono haya na kuwaangazia wengine nuru hii, kama vile katika liturujia ya Pasaka mwanga wa mshumaa huu huwasha mishumaa mingine mingi. **Imani inarithishwa,** kwa kusema, kwa kuwasiliana **kutoka kwa mtu hadi kwa mtu kama mwali wa moto unaowasha moto mwingine.**

Lumen fidei 37

Tunapofahamu mwonekano wa Mungu ndani ya kila kinachoishi, moyo hupata shauku ya **kumwabudu Bwana kwa ajili ya viumbe vyake vyote na pamoja navyo.**

Laudato Si' 87



**Mbele ya Moyo wa Kristo, ninamwomba Bwana** awe na huruma kwa mara nyingine tena kwa ajili ya ulimwengu huu uliojeruhiwa ambao alitaka kuishi kama mmoja wetu. Kwamba aeneze hazina ya nuru yake na ya upendo wake, **ili ulimwengu wetu**, unaosalia katikati ya vita, kukosekana kwa usawa kijamii na kiuchumi, ulaji na matumizi ya teknolojia dhidi ya wanadamu na **kuweza kugundua tena kile ambacho ni muhimu zaidi na cha lazima zaidi : moyo.**

Dilexit nos 31

**Ikiwa muziki wa Injili utaacha kutikisika matumboni mwetu, tutakuwa tumepoteza furaha** inayomiminika kutoka katika huruma, **upendo** unaozaliwa kutoka katika imani, **uwezo wa upatanisho** unaopata chanzo chake katika kitendo cha kujua kwamba daima tunasamehewa na kutumwa.

Ikiwa muziki wa Injili utaacha kusikika majumbani mwetu, viwanjani mwetu, katika maeneo yetu ya kazi, katika siasa na uchumi, tutakuwa tumezima melodia inayotusukuma kupigania utu wa kila mwamume na kila mwanamke. Wengine wanajinywesha kwenye vyanzo vingine. Kwetu sisi, **chanzo hiki cha utu wa binadamu na cha undugu kinapatikana katika Injili ya Yesu Kristo.**

Fratelli Tutti 277

Nasisitiza…kusaidia maskini kwa fedha inatakiwa daima kuwa suluhu la muda ili kukabiliana na dharura. Lengo kuu daima linapaswa kuwa kuwawezesha kuwa na maisha bora kupitia kazi. Fratelli Tutti 162

# Mei, mwezi wa MARIA

Mwenyeheri Petro Vigne anatualika kuishi mwezi huu kwa kustaajabia na kumwomba Bikira Maria kwa imani. *« …Mheshimuni yeye ambaye Mungu anamtukuza kuliko viumbe vyote, yeye aliye na hadhi ya kwanza katika ulimwengu wote, yeye ambaye kwa kumwiga Mwanawe mpendwa, amejawa na huruma kwa ajili ya wadhambi…*

*Anajitolea kutusikiliza vizuri, kutulinda, na kututangulia kwa kila jambo tunalomwomba…»* H.N. 1-214 Tunamkabidhi mkutano ujao wa makadinali, Papa atakayechaguliwa na Kanisa zima.

***Ee Mama, tusaidie imani yetu !***
*Panda ndani ya imani yetu furaha ya Mfufuka.*
*Tukumbushe kwamba anayeamini kamwe hayuko peke yake.*
*Tufundishe kutazama kwa macho ya Yesu,*
*Ili iwe nuru katika njia yetu… L.F.60*
*Bikira na Mama Maria,*
***Uliwakusanya wanafunzi katika kutazamia Roho***
*ili kwamba lizaliwe Kanisa la uinjilishaji.*
*Utujalie sasa*
*ari mpya ya wafufuka*
*ili kuleta kwa wote Injili ya uzima*
*inayoshinda kifo.*
*…utuombee. Amina. **Aleluya** ! E.G.288*



**8 MEI : SIKUKUU**
**Ya mama yetu wa Ekaristi Takatifu**

Ambaye sisi pia tunamkabidhi **Mkutano Mkuu ujao wa Shirika** huko Valence (Ufaransa)

# Juni, mwezi wa MOYO MTAKATIFU wa YESU



Picha-sala ya Petro Vigne

*Katika ensiklika yake ya mwisho, Papa Fransisko anasema:*

*“ **Ibada kwa Moyo wa Kristo** hatua kwa hatua ilipita zaidi ya maisha ya utawa **na kujaza hali ya kiroho mabwana watakatifu, wahubiri na waanzilishi wa mashirika ya kitawa** ambao waliieneza hadi maeneo ya mbali zaidi ya dunia. D.E 112»*

Petro Vigne, Mwanzilishi wetu, alituonesha jinsi Sakramenti Takatifu, Ekaristi, ilivyo zawadi ya thamani ya upendo wa Moyo wa Yesu, Moyo wa kibinadmu na wa kimungu. *« Mwanadamu hajui wapi ilipo hazina yake…kwa hiyo ni lazima nikuambie mahali wema huu thabiti ulipo. Hazina ya wanadamu wote ni YESU katika Ekaristi Takatifu, na kilicho cha thamani zaidi ndani yake ni Moyo wake Mtakatifu…Moyo ukiwa ni sehemu tajiri zaidi ya mwanadamu, je ni mdogo katika Mwili wa Mwokozi ?… Ee Moyo Mtakatifu wa Yesu, ninakuabudu kwa hivyo, kama hazina yangu, na **wema wangu wote katika chanzo chake**… Ni nani asiyempenda Yule atupendaye kwa upole namna hii ? H-N.»* mwaliko wa kweli wa kurudi karibu na Moyo wa Yesu.